**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**664** **MITAALA NA UFUNDISHAJI**

**Muda: Saa 3.** **17th November 2004**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu **B** na swali **moja (1)** kutoka sehemu **C**.
3. Sehemu **A** ina alama 36, sehemu **B** ina alama 40 na sehemu **C** ina alama 24.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 36)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza maana ya usimamizi wa mitaala shuleni.
2. Tofautisha kati ya mtaala wa kitaifa na ule wa kimataifa.
3. Eleza umuhimu wa kushirikisha wadau katika kutathmini mitaala.
4. Taja hatua muhimu za kupanga ratiba ya masomo.
5. Eleza mchango wa walimu katika kubuni nyenzo za kujifunzia.
6. Kwa nini ni muhimu kufanya utafiti kabla ya kuanzisha mtaala mpya?
7. Eleza namna elimu ya maadili inavyoweza kuingizwa kwenye mitaala ya shule.
8. Fafanua dhana ya ufuatiliaji wa elimu.
9. Eleza namna mwalimu anaweza kuwasaidia wanafunzi wenye uwezo mdogo wa kuelewa.

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **mawali (2)** katika sehemu hii.

10. Jadili nafasi ya tathmini katika kubaini mafanikio ya utekelezaji wa mitaala.
11. Eleza umuhimu wa kutumia vifaa vya TEHAMA katika kufundisha.
12. Jadili athari za ukosefu wa uwiano kati ya nadharia na vitendo katika elimu.
13. Eleza mchango wa viongozi wa shule katika kuhakikisha utekelezaji bora wa mitaala.

## SEHEMU C (Alama 24)

Jibu swali **moja (1)** katika sehemu hii.

14. Eleza faida za kufanya tathmini ya pamoja kati ya mwalimu na mwanafunzi.
15. Jadili umuhimu wa ubunifu katika kufundisha masomo ya vitendo.
16. Eleza namna ushirikiano wa walimu na jamii unavyoweza kuongeza ubora wa elimu.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org